JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MWONGOZO WA UJENZI NA UENDESHAJI WA VYOO VYA UMMA KATIKA HALMASHAURI YA JIJI DODOMA

October 2021

MWONGOZO WA UJENZI NA UENDESHAJI WA VYOO VYA UMMA KATIKA HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

A. UTANGULIZI

Vyoo vya Umma ni majengo/vyumba vinavyopatikana katika maeneo ya umma kwa lengo la matumizi ya kukusanya moja kwa moja taka za binadamu (kinyesi na mkojo) na kuzitupa taka hizo kupitia njia/mfumo unaokubalika.

Maeneo ya Umma ni masoko, vituo vya magari/ stendi, gulio, minada, maeneo ya wazi/maeneo ya mapumziko, ofisi, shule n.k.

Vyoo vya umma vipo sehemu nyingi kwa lengo la kutoa huduma inayostahili kwa wateja, wasafiri, wagonjwa, watalii na jamii kwa ujumla kulingana na bidhaa au huduma inayotolewa. Usafi ni moja ya vitu vinavyopewa kipaumbele ili mteja asijiulize wapi anapotimiza haja zake.

Vyoo salama na vilivyo bora vyenye vifaa sahihi vya kunawia mikono baada ya kuvitumia, kwa pamoja, husaidia kuzuia magonjwa mengi yatokanayo na vijidudu vilivyomo katika kinyesi cha binadamu. Vyoo na mifumo ya uondoaji na uhifadhi wa kinyesi iliyojengwa vibaya ni vyanzo vikuu vya magonjwa na uchafuzi wa mazingira na maji yaliyoko chini ya ardhi.

Uondoaji na hifadhi salama wa kinyesi kwa kujenga, kutumia na kutunza vyoo kwa usahihi, pamoja na matumizi sahihi ikiwa ni pamoja na kunawa mikono kwa maji safi, tiririka na sabuni baada ya kujisaidia,

huzuia ueneaji wa vijidudu vinavyosababisha magonjwa na ni mahitaji ya msingi kwa ajili ya afya ya binadamu.

Lengo la Mwongozo

Lengo la Mwongozo huu ni kuboresha utaratibu unaotumika hivi sasa kwenye Halmashauri ya Jiji katika ujenzi, usimamizi na uendeshaji wa vyoo vya Umma. Aidha, mwongozo utafuatwa kwa kutazingatia Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo.

Walengwa wa Mwongozo

Walengwa wa Mwongozo ni Halmashauri ya Jiji la Dodoma, wadau mbalimbali wanaoshughulika na ujenzi wa vyoo, waendelezaji, wawekezaji na wadau wengine wa sekta ya ujenzi wa vyoo vya umma katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Matokeo ya kuwepo kwa Mwongozo

Utaratibu wa kutoa vibali vya ujenzi wa vyoo vya Umma na usimamizi wa kwenye Halmashauri ya Jiji la Dodoma utaimarishwa kama ifuatavyo:-

1. Muda wa kutoa vibali vya ujenzi wa vyoo na urasimu utapunguzwa na kuweka mazingira mazuri yanayowavutia wawekezaji wanaotaka kutoa huduma hii ya vyoo vya Umma.
2. Jiji la Dodoma litakuwa na Mwongozo mmoja ambao utatumika katika kutoa vibali vya ujenzi wa vyoo vya Umma na kusimamia ukaguzi wa ujenzi wa majengo hayo ya vyoo kwa ukaribu.
3. Kutaboresha uwepo wa vyoo vya Umma katika maeneo yasiyo na huduma hiyo na maeneo yenye uhitaji wa huduma hiyo na;

kupunguza/kuondoa uwezekano wa kutokea kwa magonjwa ya mlipuko.

Umuhimu wa vyoo vya umma

Kuzuia magonjwa: kuzuia uchafuzi wa chakula, maji na watu kutokana na kinyesi na nzi ambavyo kawaida ni vyanzo vya magonjwa kama kipindupindu, kuhara, minyoo ya safura, homa ya matumbo (taifodi) na amiba.

Kulinda uchafuzi wa vyanzo vya maji.

Chanzo cha mapato kwa Halmashauri.

Kurahisisha huduma kwa Jamii.

UMUHIMU WA KUWA NA MWONGOZO

Halmashauri ya Jiji la Dodoma imeendelea kukua kwa kasi kubwa baada ya serikali kuhamia Dodoma ambapo inaendana na ongezeko kubwa la wakazi na shughuli za kibinadamu. Aidha, halmashauri imekuwa ikitenga maeneo ya huduma za kijamii kama D center, C center, stendi na maeneo ya wazi.

Kwa utaratibu uliokuwepo maeneo haya yaliweza kugawiwa wafanyabiashara bila ya kuwepo kwa mpango mahususi ya ujenzi wa miundombinu ya vyoo. Hivyo, baadhi ya maeneo yamekuwa na wafanyabiashara na wananchi wanaoendelea na shughuli za ujasiriamali bila uwepo wa vyoo kinyume na Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2009 pamoja na Sheria ya Mazingira namba 20 ya mwaka 2004.

Kutokana na kutokuwepo kwa huduma ya vyoo kumesababisha wananchi na wafanyabiashara kujisaidia hovyo ambapo kunaweza kusababisha magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu na kuhara.

Wadau mbalimbali wamekuwa wakituma maombi ya kujenga vyoo katika maeneo hayo ambayo yanamilikiwa na Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa masharti yatakayowekwa na Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Mahali panapofaa kujenga choo

Wakati wa kufanya maamuzi ya kujenga choo linatakiwa kuangaliwa eneo ambalo halitachafua visima au vyanzo vya maji na maji yaliyopo ardhini. Hatari ya maji ya ardhini kuchafuliwa inategemea na hali ya mahali husika. Mfano aina ya udongo, hali ya unyevunyevu na umbali wa tabaka maji kutoka usawa wa ardhi.

Mahitaji ya Jamii

Huduma ya vyoo vya umma hutolewa kusaidia shughuli za afya na burudani katika mbuga na hifadhi zilizotenguliwa katika halmashauri yote.

Vyoo vya umma kwa ujumla viko kwenye sehemu za wazi za umma

Uhitaji wa vyoo vya umma umedhamiriwa kwa kutumia kanuni, majukumu na viwango vya utoaji vilivyoainishwa katika Mkakati wa Nafasi ya Wazi ya Umma (POS).

Jiji litajulisha au kushauriana na jamii juu ya kufunga, kukarabati na kuondoa vyoo vya Umma.

Vyoo vya umma vitazingatiwa tu katika eneo la wazi la mkoa, wilaya au jamii ikiwa kuna kiwango cha kutosha cha mahitaji ya jamii

Maeneo yanayofaa kwa vyoo vya Umma

Vyoo vya Umma vitajengwa katika maeneo yote ya Umma (Public area) ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma ambayo yametengwa na kupimwa mahususi kwa huduma za kijamii.

Sifa za jumla za vyoo vya Umma

- Vyoo vya Umma lazima viwe vimetenganishwa kwa jinsia zote mbili (wanawake na wanaume).
- Kuwe na choo maalumu kwa ajili ya watu wenye ulemavu.
- Vyoo vya wanaume lazima viwe na sehemu ya haja ndogo (urinals).
- Vyoo vya wanawake lazima viwe na chumba maalumu kwa ajili ya kubadilishia nguo/taulo za kike pamoja na kifaa maalumu cha kuhifadhi taka za hedhi.
- Kuwe na vigae 'tiles' sakafuni kote na kutani. Vigae visiwe chini ya 1.5m urefu.
- Pande zote mbili wanawake na wanaume kuwe na masinki na sabuni za maji kwa ajili ya kunawia mikono.
- Kuwe na vifaa vya kutunzia taka katika pande zote mbili.
- Kuwe na stoo kwa ajili ya kutunzia vifaa vya usafi.
- Vyoo vyote vya umma vinapaswa kujumuishwa kwenye ratiba ya usafi ya halmashauri.

- Kuwe na huduma za bafu kwa jinsia zote (wanawake na wanaume)
- Wafanyakazi wote/wahudumu wote wapimwe afya na wapewe elimu ya afya.
- Njia za kuzima moto zinatakiwa kuwekwa, ikiwezekana kwa vyoo vyote vya Umma katika halmashauri.
- Nyakati za ufunguzi kwa ujumla zitakuwa kutoka 12:00 asubuhi hadi 3:00 usiku isipokuwa uongozi umeamua vingine kulingana na uhitaji kama stendi ambapo huduma utolewa masaa 24.
- Vyoo vya Umma havipaswi kufunguliwa usiku kucha ili kuzuia tabia isiyofaa na uharibifu miundombinu.
- Tanki za kuhifadhia maji [simtank] katika kuhakikisha uwepo wa maji muda wote iwapo uhaba wa maji utajitokeza.
- Kuwepo kwa ofisi ya kutolea huduma ya choo cha Umma.

HUDUMA YA VYOO VYA UMMA KATIKA JIJI

Katika sehemu za mijini, matatizo ya kiafya yanaweza kuenea haraka sana. Siyo rahisi kuboresha huduma za vyoo katika miji yenye msongamano wa watu wengi bila msaada mkubwa wa serikali, asasi na wadau wengine.

UENDESHAJI WA VYOO VYA JIJI

Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa sasa ina mifumo inayo simamia uendeshaji wa vyoo vya Umma.

Vyoo vya Umma vilivyojengwa na halmashauri.

Mfumo wa uendeshaji wa vyoo vya Umma vilivyojengwa na halmashauri kwa sasa vinaendeshwa na watu binafsi ambao wamepewa Mashine za Kielektroniki za kukusanyia mapato (POS) za halmashauri. Fedha inayokusanywa inaingizwa moja kwa moja kwenye akaunti ya Halmashauri ya Jiji na baada ya hapo muendeshaji hupewa 30% ya makusanyo yote. Gharama zote za uendeshaji hufanywa na muendeshaji mwenyewe.

Vyoo vya Umma vilivyojengwa na wadau

Mfumo wa uendeshaji wa vyoo vya umma vilivyojengwa na wadau kwa sasa havitumii (POS) na mmiliki hupewa mkataba wa miaka kadhaa ya undeshaji, baada ya miaka hiyo kuisha choo hicho kitaanza kumilikiwa na Jiji hivyo aliyekijenga anaweza kuwa mpangaji kwa maana ya kwamba atapewa mashine ya POS na atapewa 30% ya makusanyo yote.

MAPENDEKEZO YA MFUMO WA UENDESHAJI WA VYOO VYA UMMA

Katika kukabilina na upungufu wa vyoo katika baadhi ya maeneo ya umma kama minada,magulio n.k mwongozo huu unatoa fursa kwa wadau mbalimbali kuweza kuunga mkono juhudi za Halmashauri katika kuboresha miundombinu ya vyoo katika maeneo ya Umma kwa lengo la kukabiliana na magonjwa ya milipuko katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma kuboresha mandhari na usafi wa mazingira.

Katika Mwongozo wa uendeshaji wa vyoo vya Umma yanapendekezwa mambo yafuatayo:-

1. Jiji litaendelea kujenga vyoo katika maeneo mbalimbali ya Umma kwa kadri itakanyowezekana. Aidha, uendeshaji wa vyoo hivi utaratibiwa kwa utaratibu utakaoamuliwa na Halmashauri kwa wakati huo. Mfumo huu utatoa fursa ya Jiji kusimamia moja kwa moja makusanyo yatokanayo na vyoo hivi au kuweka mzabuni atakayekusanya ada ya matumizi ya huduma za vyoo kama itavyoamuliwa na Halmashauri.

2. Mwongozo unatoa fursa kwa wadau mbalimbali watakaohitaji kujenga vyoo vya Umma katika maeneo yaliyotengwa na kupimwa mahususi kwa shughuli za umma kwa kuzingatia mchoro utakaotolewa na Ofisi ya Mhandisi wa Halmashauri ya Jiji na kufuata sifa za vyoo vya Umma. Kuwepo kwa Makubaliano maalumu kati ya Halmashauri na mdau (MoU).

3. Katika makubaliano ya awali mgawanyo wa mapato yatakayopatikana kila mwezi baada ya ujenzi uwe wa asilimia 40% kwa Jiji na asilimia 60% kwa mdau kwa kipindi cha miaka 10. Baada ya kipindi hicho, choo kitakuwa mali ya Halmashauri na Mhusika anaweza kuingia mkataba utakaokuwa unatumika kusimamia na kuendesha vyoo vya Umma vilivyojengwa na kusimamiwa na halmashauri.

UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI KWA WAOMBAJI BINAFSI

Mhusika, mdau au Kampuni inayohitaji kujenga vyoo vya Umma katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma itawajibika kufuata utaratibu ufuatao:-

1. Kuandika barua ya maombi kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma kupitia kwa mtendaji wa Kata husika ambaye ataipitisha baada ya kujiridhisha kuwa eneo analoomba ni mahusisi kwa huduma hiyo.
2. Kujaza fomu maalumu ambayo itapitishwa katika idara zote zinazohusika katika Mamlaka ya Upangaji.
3. Kuingia Mkataba wa makubaliano (MoU) na Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa ajili ya ujenzi na uendeshaji wa Vyoo vya Umma .

KAMATI MAALUMU YA WATAALAM

Kutakuwepo na Kamati maalum ya wataalam yenye wajumbe kutoka idara zifuatazo kulingana na utaalam zao:

I. Idara ya Mipango Miji, Ardhi na Maliasili

II. Idara ya Ujenzi

III. Idara ya Mazingira na uthibiti wa taka ngumu

IV. Idara ya Afya (inashauriwa kuwa Afisa Afya)

V. Mtendaji wa Kata husika ambapo ujenzi utafanyika.

MAJUKUMU YA KAMATI

I. kupitia na kuchambua maombi yote yaliyowasilishwa kwa Mkurugenzi.

II. Kufanya ukaguzi wa eneo aliloomba mhusika kwa ujenzi wa vyoo vya Umma na kuandika taarifa ya kina.

III. Kuhakikisha uwepo wa michoro ya vyoo vya Umma vinavyolingana na uhalisia na mazingira halisi.e.g maeneo ya mnada na maeneo ya starehe.

IV. Kumshauri Mkurugenzi wa Jiji kitaalamu hatua za kuchukua iwapo mhusika amekidhi au kutokidhi vigezo.

Utekelezaji na usimamizi wa Mwongozo

Wadau na Wataalamu mbalimbali wa Halmashauri watahusishwa na kushiriki moja kwa moja katika usimamizi na utekelezaji wa Mwongozo huu kwa mujibu wa Taaluma zao

MATUMIZI

Mwongozo huu utatumika katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma baada ya kupitishwa na kuidhinishwa na vikao halali vya Halmashauri .

HITIMISHO

Mwongozo huu ukitekelezwa kikamilifu utaboresha mazingira ya uwekezaji katika utoaji wa huduma ya vyoo ambapo utarahisisha kupata kibali cha ujenzi wa vyoo vya Umma bila kuathiri sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Pia, utaimarisha taratibu za ukaguzi na usimamizi na uwajibikaji katika ngazi zote za Halmashauri kwa ujenzi wa majengo ya vyoo vya Umma katika Halmashauri kwa kuzingatia matakwa ya Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo. Aidha, kwa kuzingatia matakwa ya Mwongozo huu huduma za Vyoo vya Umma itaboreshwa katika maeneo ya minada, maeneo ya wazi na maeneo mengine ya Umma na kuondoa kero ya baadhi ya wananchi kujisaidia hovyo katika maeneo yasiyo na vyoo vya Umma. Mwongozo huu utasaidia kuweka uwazi, uwajibikaji na kurahisisha ufuatiliaji kwa mamlaka mbalimbali za halmashauri.

Mwongozo huu ni kama ulivyojadiliwa na kupitishwa na kikao cha baraza la madiwani wa halmashauri ya Jiji la Dodoma cha tarehe 27/10/2021.

Joseph.C Mafuru
MKURUGENZI WA JIJI
JIJI LA DODOMA

MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA
S.L.P. 1249,
DODOMA

Mhe Prof Davis Mwamfupe
MSTAHIKI MEYA
JIJI LA DODOMA

HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA
FOMU YA MAOMBI YA UJENZI NA UENDESHAJI WA CHOO CHA UMMA

A. TAARIFA ZA MWOMBAJI

i) Jina la kwanza: .....Jina la Kati:.....Jina la Mwisho:.....

ii) Makazi ya Mwombaji Mtaa.....Kata .....

iii) Jinsi: Me /Ke.....

iv) Barua pepe: .....

v) Namba ya Simu:.....

vi) TIN:.....

vii) Aina ya Kitambulisho:.....

viii) Namba ya kitambulisho:.....

B: MAHALI LILIPO ENEO

i) Mtaa :.....Kata :.....Halmashauri:.....

ii) Matumizi Kwa sasa .....

iii)Jina Maarufu.....Eneo limepimwa? Ndiyo/ Hapana

IV Namba ya Kiwanja:..... Kitalu:.....

I. Matumizi ya Eneo : Eneo la Wazi/Mnada/Soko /Stendi na Biashara Nyingineyo (taja).....

C) **UTHIBITISHO WA MAELEZO YA SEHEMU B- MTENDAJI WA KATA**

Mimi Mtendaji wa Kata ya ..... nathibitisha kuwa kuna uhitaji wa huduma hiyo na taarifa zilizotolewa Sehemu "B" ni za kweli na panastahili/Hapastahili kupatiwa kibali cha kujenga choo cha Umma katika eneo hilo.

Jina.....Saini:.....Tarehe:.....

D. UTHIBITISHO WA MAELEZO- AFISA AFYA JIJI

Kwa Matakwa ya sheria ya afya ya jamii ya mwaka 2009 nimekagua na kuthibitisha kuwa eneo hilo linafaa kwa ujenzi wa choo cha Umma kwa mujibu wa sheria.

Kamili:.....Cheo:.....Saini:.....

Tarehe:.....

E. UTHIBITISHO WA MAELEZO- IDARA YA MAZINGIRA

Kwa matakwa ya Sheria ya Mazingira namba 20 ya mwaka 2004. Nimekagua na kuthibitisha kuwa eneo hilo linafaa kwa ujenzi wa choo cha umma kwa mujibu wa sheria.

Kamili:.....Cheo:.....Saini:.....

Tarehe:.....

F. UTHIBITISHO WA MAELEZO- IDARA YA MIPANGO MIJI

kwa mahitaji ya kiafya, usalama na hifadhi ya mazingira. Mahitaji ya miundombinu iliyopo kama udongo, mfumo wa mifereji ya maji ya mvua, usalama dhidi ya majanga ya moto, na mabadiliko ya tabianchi, utumiaji endelevu wa nishati, mahitaji ya Mipango Miji, n.k (Kifungu 29 (3) cha Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya Mwaka 2007). Eneo linafaa kwa mahitaji ya ujenzi wa choo cha Umma

Kamili:.....Cheo:.....Saini:.....

Tarehe:.....

E. UTHIBITISHO WA MAELEZO- IDARA YA UJENZI

kwa mujibu viwango vilivyoanishwa kwenye Sheria ya Mamlaka ya Serikali ya Mitaa Sura 288 na Kanuni ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) (Udhibiti Uendelezaji) ya Oktoba, 2008 (GN No. 242); kibali kinaweza kutolewa/hakitatolewa kwa Ujenzi wa Choo cha Umma katika eneo tajwa hapo juu

Kamili:.....Cheo:.....Saini:.....

Tarehe:.....

E. MAONI YA - TIMU YA WATAALAMU

Baada ya Timu ndogo ya Wataalamu(Scrutinization Team) ya uidhinishaji wa vibali vya ujenzi wa vyoo vya Umma kufanya ukaguzi wa eneo husika pamoja nyaraka za maombi kwa mujibu wa Mwongozo huu. Timu inamshauri Mkurugenzi **kutoa/kutotoa** idhini ya ujenzi wa choo cha umma katika eneo lililoombwa.

Jina.....
Saini.....
Katibu wa Timu

Jina .....
Saini .....
Mwenyekiti wa Timu

F: IDHINI YA HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

Kibali kinatolewa /hakitatolewa kulingana na ushauri wa walaamu, taratibu ziendelee/Zisiendelee kwa kujibu wa sheria

Maoni/Maelelezo .....
.....
.....
.....
.....
Jina :.....
Cheo:.....
Saini:.....
Tarehe:.....